

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI
KILICHOFANYIKA TAREHE 12/3/2022 KATIKA OFISI YA
KITENGO CHA MANUNUZI.

MAHUDHURIO:

- | | |
|---------------------------|------------|
| 1. Ndg. Ramadhani Y.Marwa | Mwenyekiti |
| 2. Ndg.Ramadhani Salum | Katibu |
| 3. Ndg Revocatus Joseph | Mjumbe |
| 4. Ndg. Meishack Libent | Mjumbe |

SECRETARIETI WALIOHUDHURIA:

- | | |
|-------------------------|--------------|
| 1. Ildephonce Valentine | Sekretarieti |
|-------------------------|--------------|

WASIHUDHURIA

1. Ndg.Mayala P.Sengerema
2. Dr.Deocles Ngaiza

AGENDA:

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia dondoo.
3. Kutoa kibali cha matumizi ya fedha za miradi ya Elimu Msingi, Elimu Sekondari, Afya na mradi wa jengo la Utawala kwa kutumia forece Account.
4. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa tarehe 14/12/2021
5. Kufunga kikao.

1.Kumb. NA .../2021/2022 - KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwakaribisha wajumbe wa bodi ya zabuni pamoja na Secretariat ya Manunuzi kwenye kikao maalum cha Bodi ya Zabuni. Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa kikao hiki kinagusa miadi wa Ujenzi wa jengo la Utawala, Nyumba ya watumishi 3 in 1 Afya, Ujenzi wa madarasa 24 ya Elimu S/Msingi, Ujenzi wa madarasa 85 Elimu Sekondari mazingira na uzoaji wa takangumu. Alieleza kuwa miradi hii inahitaji kujadiliana kwa makini ili kupata mwelekeo utakao leta tija kwenye Taasisi. Baada ya utangulizi huo Mwenyekiti alifungua kikao saa 06.15mchana.

2.Kumb. NA .../2021/2022 - KURIDHIA DONDOO.

Katibu aliwapitisha wajumbe kwenye dondoo zilizokuwa zimeandaliwa ziko sawa na zituongoze katika kikao hicho.

3.Kumb. NA .../2021/2022 - KUTOA KIBALI CHA MATUMIZI YA FEDHA ZA MIRADI YA ELIMU MSINGI, ELIMU SEKONDARI, AFYA NA MRADI WA JENGO LA UTAWALA KWA NJIA YA FORCE ACCOUNT.

Katibu aliwapitisha wajumbe kwenye maombi yaliyowasilishwa ya kuomba kibali cha kutumia force account kwa miradi hiyo kwani muda uliopo ni mdogo kuligana na maelkezo yaliyotolewa na Wizara ya Tamisemi na kazi hizo zifanyike kwenye ngazi ya chini wakisimamiwa na wataalam kutoka kwenye Ofisi ya Mkurugenzi. Katibu alibainisha miradi hiyo kwa kutaja kila aina ya mradi na fedha zake kama ifatavyo-

- A). Ujenzi wa Jengo la Utawala kwa gharama ya 1,000,000,000.00.
- B). Ujenzi wa shule shikizi za Msingi saba zenye vyumba 24 vya madarasa thamani yake 480,000,000.00
- C). Ujenzi wa nyumba za watumishi Kituo cha Afya Murongo yenye thamani ya Tsh. 90,000,000.00
- D). Ujenzi wa wodi za wanaume na wanawake na jengo la upasuaji na nyumba ya kuifadhia maiti katika Hosipitali ya Wilaya yenye thamani ya Tshs. 800,000,000.00.

E). Ujenzi wa wodi ya wazazi, upasuaji na jengo la kufulia katika Kituo cha Afya Rutunguru yenye thamani ya Tsh. 250,000,000.00

F). Ujenzi wa madarasa 85 katika shule za Sekondari katika Wilaya ya Kyerwa zenye thamani ya Tsh. 2,200,000,000.00.

Baada ya Katibu kuwapitisha katika nyaraka zilizowasilishwa, wajumbe wote kwa pamoja walikubaliana na maombi hayo kuwa taratibu zifuatwe na wataalam kutoka ofisi ya Mkurugrni wajitahidi kuwa karibu na miradi hiyo kwani fedha hizo ni za wafadhili hivyo inzhitaji usimamizi wa kina nakuangalia thamani ya mradi iendane na ualisia wa kazi. Pia manunuzi yafanyike haraka lakini kwa kuzingatia taratibu kanuni na sheria zinazotuongoza ili kuendana na muda uliopangwa.

4. Kumb. NA .../2021/2022 –KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIAO CHA TAREHE 14.12.2021.

Mwenyekiti alimkaribisha Katibu kusoma mhtasari wa kikao kilichopita. Katibu alisoma na mhtasari huo na kisha wajumbe wakasema yaliyosomwanndiyo yaliyojadiliwa katika kikao hicho

5. Kumb. NA/2021/22-KUFUNGA KIKAO.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michangao yao na kuwatakia majukumu mema. Kikao kimefungwa mnamo saa 7.10 mchana

UMETHIBITISHWA



.....
(Ramadhani Y. Marwa)

MWENYEKITI



.....
Ramadhani Salum

KATIBU